



Kikosi cha Usimamizi wa Kesi za Ulinzi wa Mtoto Lebanon
Mwongozo kwa wafanyakazi wa kesi za Ulinzi wa watoto wa kuwashirikisha watoto au walezi
kuhusu COVID-19
Hatua za Usalama za kujikinga wakati wa kufanya Kazi ya Usimamizi wa Kesi
Machi 2020

Ulinzi wa Mtoto COVID -19 DropBox [LINK](#)

Kama Mfanyakazi wa kesi za Ulinzi wa Mtoto wakati wa mlipuko ya COVID-19, ni muhimu kuwashirikisha kikamilifu taarifa **rahisi za kisayansi**¹ na za kueleweka, kwa watoto, walezi wao na wanajamii kuhusu njia ambazo wanazoweza kujilinda wao na wapendwa wao kipindi cha mlipuko wa COVID-19.

Muongonzo huu unagusia **jinsi ya kuelezea dhana za jinsi ya kuchukua tahadhari za usalama kuwalinda wengine na wewe mwenyewe**. Taarifa katika mwongozo huu zinaweza kutumiwa wakati wa kufanya ufuatiliaji wa kesi ana kwa ana au kutokea mbali. Unaweza kutumika:

- Kivyake kwa familia ambazo unaweza kuziona kuwa kwenye hatari zaidi na hazijapata taarifa muhimu;
- Kama sehemu ya ufuatiliaji wa kesi za kawaida.

Kumbuka: *Katika maandishi mlalo hapa chini ni muhtasari wa nini cha kusema kwa watoto, walezi au wanajamii, nna katika maandishi yasiyo mlalo ni baadhi ya hatua unaweza kuchukua kama mfanyakazi wa kusimamia kesi ili kupunguza hatari.*

1. NANI NIPANGE KUMFIKIA KWANZA?

Wape kipaumbele watoto walio hatarini zaidi na familia katika kesi ulizonazo kwanza, hii inaweza kufanywa sambamba na mwongozo wa usimamizi wa kesi. Vigezo vya kutoa kipaumbele kwenye vikao vya uelimishaji kwa njia ya simu au ana kwa ana ni pamoja na (hakuna mtiririko maalumu):

- Watoto walio katika kesi ulizonazo waliotathminiwa kuwa katika hatari kubwa
- Watoto waishio na kufanya kazi mitaani ambao huzurura ikiwa ni pamoja na watoto wanaokusanya takataka
- Watoto wanaofanya kazi katika aina zote za kazi
- Watoto wasio na uangalizi na waliotengwa
- Watoto wenye ulemavu
- Watoto walioathirika na unyanyasaji wa kijinsia
- Watoto wenye matatizo ya afya ya akili
- Watoto walio na walezi wenye matatizo ya afya ya akili
- Watoto ambao wanaongoza familia

¹ *Tafadhali kumbuka yaliyomo yametolewa kutoka kweye Kituo cha **Kudhibiti na Kuzuia Magonjwa (tovuti ya CDC)** na **Shirika la Afya Duniani (WHO)**, ili taarifa ziwasaide wafanyakazi waoosimamia kesi wanaotembelea kaya na kuwaelimisha walezi nchini Lebanon kuhusu athari zinayoweza kutokana ya COVID-19 kwa watoto.

- Watoto walio na mtu katika familia mwenye maradhi sugu (maelezo yameorodheshwa hapa chini)
- Watoto walio katika kesi ulizonazo wanaoishi katika maeneo yenye msongamano wa watu ambapo kunaweza kuongeza hatari ya maambukizi kama hawafahamu jinsi ya kujikinga na kukabiliana nao kwa haraka.

2. **KUTEMBELEA MAJUMBANI**

Kutembelea ama kutokutembelea majumbani kunategemeana sana na agizo la Serikali ya Lebanon (GoL) katika ngazi ya kitaifa na ngazi za chini, pia sheria za usalama za shirika lako wakati ukizingatia ukubwa wa kesi.

Pale inapoonekana kuwa ni salama na GoL na asasi yako kutembelea majumbani, basi inashauriwa:

- 1.) **Kabla ya kufanya ziara yoyote na kila mara unapongea na familia** kwa njia ya simu, ulizia kama kuna mtu kwenye familia ambaye hajisikii vizuri. **Kama kuna mtu katika familia hajisikii vizuri, usiwatembelee nyumbani na uwashauri na kuwasaidia kupiga simu kweye namba maalumu iliyotolewa na Wizara ya Afya 76-592699** au watoa huduma wengine kulingana na njia za rufaa zilizo boreshwa.
- 2.) **Wakati wa ziara yako tumia na ELEZEA yafuatayo kwa familia na ni kwa nini unachukua tahadhari hizi na kwa nini zinapaswa kuchukuliwa.**
 - a) **Dumisha kujitenga kijamii:** weka umbali wa angalau mita 1 (hatua 3) kati yako na mtu yeyote anayekohoa au kupiga chafya.
ELEZEA kwamba kama inavyopendekezwa na Shirika la Afya Ulimwenguni wakati mtu akikohoa au kupiga chafya, hueneza matone madogo kutoka puani au mdomoni ambayo yanaweza kuwa na virusi. Ukiwa uko karibu sana, unaweza ukavuta hewa yenye matone hayo, pamoja na virusi vya COVID-19 ikiwa mtu anayekohoa ana ugonjwa.
 - b) **Osha / takasa mikono kabla, wakati wa na baada ya kila matembezi:** Safisha mikono yako mara kwa mara na kwa kutumia kitakasa mikono au kuosha kwa sabuni na maji.
ELEZEA kwamba kuosha mikono yako kwa sabuni na maji au kwa kutumia kitakasa mikono kunaua virusi ambavyo vinaweza kuwa mikononi mwako.
 - c) **Epuka kugusa macho, pua na mdomo kabla, wakati na baada ya matembezi**
FAFANUA kuwa mikono inagusa sehemu nyingi na inaweza kuchukua virusi. Mara baada ya kuchafuliwa, mikono inaweza kuhamishia virusi kwenye macho yako, pua au mdomo. Kutokea hapo, virusi vinaweza kuingia ndani ya mwili wako na vinaweza kukufanya uwe mgonjwa.
 - d) **Fuata Usafi wakati wa Upumuaji:** Hakikisha wewe na watu walio karibu nawe wanafuata hatua nzuri za usafi za upumuaji. Hii inamaanisha kufunika mdomo na pua yako na kiwiko cha mkono wako au tishu wakati unakohoa ama kupiga chafya. Kisha tupa tishu iliyotumika mara moja.
ELEZEA kuwa matone yanasambaza virusi. Kwa kufuata hatua nzuri za usafi za upumuaji, unawalinda watu walio karibu nawe mbali na virusi kama vya baridi, mafua na COVID-19.
 - e) **Vaa barakoi (mpya kwa kila matembezi) lakini zingatia kufuata yafuatayo:**
 - Kabla ya kuvaa mask, osha mikono na kitakasa mikono ama kwa sabuni na maji.
 - Funika mdomo na pua na barakoi na hakikisha hakuna upenyo kati ya uso wako na barakoi.
 - Epuka kugusa barakoi wakati umeivaa; ukifanya hivyo, osha mikono yako na kitakasa mikono ama kwa maji na sabuni.
 - Badilisha barakoi mara tu inapoloa na usitumie tena barakoi zitumikazo mara moja tu.

- Kuvua barakoi: itoe kutokea nyuma (usiguse sehemu ya mbele ya barakoi); tupa mara moja kwenye pipa lililo fungwa; osha mikono na kitakasa mikono ama kwa maji na sabuni.
- ELEZEA** unavaa barakoi kwa sababu ya kazi a majukumu yako, lakini kama upo mzima wa afya:
- Unahitaji tu kuvaa barakoi kama unaumwa, unakohoa au kupiga chafya na kama unamuhudumia mtu ambaye ni mgojwa au anayeshukiwa kuwa na COVID-19.
 - Vibarakoi vinafanya kazi vizuri pale vinapotumiwa kwa usahihi na kwa kushirikiana na kunawa mikono mara kwa mara kwa kutumia kitakasa mikono ama kwa maji na sabuni.

Tafadhali Kumbuka:

- **Kama haujisikii vizuri, usitembelee majumbani na usiende kazini na ubakie nyumbani.** Kama unahoma, unakohoa ama unapumua kwa shida, tafuta matibabu na upige simu mapema. **Kama** imethibitishwa una COVID -19, watu wote wa nyumbani kwako wanapaswa kubakia karantini kwa angalau siku 14. Hii ni hatua ambayo inakuinga wewe, familia yako na jamii yako.

3. NAWEZAJE KUWAFIKIA WATOTO WALIO KATIKA KESI ZANGU HIVI SASA AMBAPO SIWEZI KUWATEMBELEA MAJUMBANI?

- Ikiwa umepewa maelekezo na serikali ya Lebanon ya kuacha mizunguko yote nchini, ni muhimu kwamba **asasi zinazoshughulikia ulinzi wa mtoto kuweka kipaumbele katika kuwasiliana na familia kwa njia ya simu kufanya usimamizi wa kesi na ikiwa inafaa waelimisha juu ya COVID-19.**

4. MUHTASARI WA KUTUMIA WAKATI WA KUTEMBELEA na / au KUWASILIANA NA FAMILIA KWA NJIA YA SIMU KWA UJUMBE MAHUSUSI JUU YA COVID-19:

Tafadhali kumbuka **anza kufanya uelimishaji na mzazi / mlezi pale tu inapofaa.** Ni muhimu wasimamizi wa kesi za ulinzi wa mtoto, kuzingatia kama mzazi / mlezi yupo, kama wanaweza kuwashirikisha taarifa watoto wanaowatunza na kama wanaweza kuchukua tahadhari za msingi. Kama kulingana na uzoefu wako unafahamu kwamba mzazi / mlezi hayupo na hana uwezekano wa kuchukua hatua kumlinda mtoto anayesimamiwa kesi, tafadhali fanya hivyo na mtu wa karibu zaidi anayeweza kuchukua tahadhari za msingi za kiafya kwa mtoto, na jamii. Kwenye baadhi ya kesi, huyu anaweza kuwa mtoto ambaye unamsaidia.

Habari, Mimi ni _____ kutokea _____. Je, huu ni muda mzuri wa kukupigia simu?

Utakuwa na kama dakika 20 tupitie pamoja baadhi ya mambo kuhusu virusi vya COVID - 19?

Habari juu ya virusi vya COVID - 19 ziko kila mahali, tunafahamu kuwa kwa baadhi hii inaweza kuwaelemea, lakini tunataka ujue kuwa tuko hapa kukusaidia na hakikisha una habari sahihi.

Katika wakati huu serikali ya Lebanon, Umoja wa Mataifa na Asasi za Kiraia (Kama, weka jina la shirika lako) zinajaribu kufuatilia maelekezo ya wataalamu wa Afya ya kubakia ndani na kuzuia mizunguko yote ikihusisha ushiriki kwenye shughuli za kijamii kama kukutana na marafiki, harusi, mazishi, michezo n.k. Sababu ya kutakiwa kufanya hivyo ni kuzuia maambukizi ya COVID-19 ili kuwalinda watu walio katika hali hatarishi katika jamii zetu kwa ujumla. Manispaa yako (kupitia afisa polisi wa manispaa) na viongozi wa kijamii inawezekana wamekutaka kufanya hivyo pia, na hili ni kwa kila mtu bila kujali utaifa au historia.

Kama mzazi / mlezi wa kiume au wa kike wa (majina ya mtoto / watoto, ni muhimu wewe kuwa sawa na taarifa juu ya COVID - 19 ili uwe tayari kuchukua hatua na kujua jinsi ya kusimamia pale ambapo mtu katika jamii yako au kaya anashukiwa au anaogua COVID - 19.

Hizi ni taarifa nyingi kuzielewa (na kukushirikisha taarifa hizi kwa simu sio vyema) lakini kwa kuzingatia hali iliyopo hii ndio njia bora tunayoweza kufanya kwa sasa. Ninafuraha kukusaidia kufanya kikao cha uelimishajii na (majina ya mtoto / watoto) na watoto wako wengine lakini ningependelea kuanza na wewe kwanza.

Kama sehemu ya kampeni yetu ya uelimishaji wakati wa COVID-19, tunataka kuhakikisha kama familia mnapata taarifa mpya kuhusu COVID-19. Sisi pia tunajifunza juu ya COVID-19 kwa hivyo tutahakikisha kadri tunapopokea taarifa mpya, tunakushirikisha na wewe. Tungependa kukushirikisha:

- 1) Hatua za vitendo za kujikinga ambazo unaweza **kutekeleza mwenyewe, katika familia yako na jamii**
- 2) **Nani wa kuwasiliana naye** pale wewe, mtu katika familia yako, au katika jamii akionyesha dalili kama za mafua: homa, uchovu, kikohozi, kupumua kwa shida au maumivu ya misuli
- 3) Nini cha kuzingatia kama familia na wanajamii wengine **hatua tofauti unazoweza kuchukua kujiandaa** ikiwa mtu apatwa na ugonjwa au ni mgonjwa katika familia yako

ULIZA: Je! Unaweza kuniambia kidogo juu ya kile ulichokisikia juu ya COVID-19 na kutoka kwa nani?

Kumbuka: Chukua muda kumsikiza mlezi au mtoto ili kutathmini ikiwa wamepata taarifa za kutosha / za usahihi. Kama wamepata taarifa za kutosha au wanahisi kuwa wana habari za kutosha / sahihi na hawana imani potofu unaweza kuendelea kuelezea yafuatayo kuhusu virusi vya COVID - 19.

Fafanua tena: Nitafanya, kila ninachoweza kukushirikisha taarifa ambayo tumepokea kutoka kwa vyanzo vya afya vya kuaminika vya kimataifa, kama vile Shirika la Afya Duniani. **Mimi si mtaalamu wa huduma za afya**, na taarifa zinabadilika kila mara. Tafadhali niulize maswali yoyote na nataka ufahamu ikitokea kuna kitu ambacho sina nacho, nitarejea kwako baada ya kuangalia kwenye chanzo rasmi.

Kwanza, wacha nieleze COVID-19 ni nini: **COVID-19 ni ugonjwa wa kuambukiza unaosababishwa na virusi vipya vya coronavirus viliyogunduliwa hivi karibuni baada ya kuzuka nchini China.**

Sasa NITAELEZEA JINSI YA COVID-19 INAVYOENEZWA, COVID-19 Inaenea:

- **Watu wanaweza kupata COVID-19 kutoka kwa watu wengine ambao wana virusi.** Ugonjwa unaweza kusambaa kutoka kwa mtu mmoja hadi kwa mtu mwingine kupitia matone madogo kutoka kwenye pua au mdomo ambayo husambazwa pale mtu mweye maambukizi ya COVID-19 aapokohoa au kutoa hewa nje. Matone haya huangukia kwenye vitu na sehemu zinazomzunguka mtu.
- **Watu wengine wanakuja kupata COVID-19 kwa kugusa vitu na sehemu hizo, kisha kugusa macho yao, pua au mdomo.**
- **Watu wanaweza pia kupata COVID-19 ikiwa watawuta hewa yenye matone kutoka kwa mtu aliye na COVID-19 ambaye ana kohoa au kutoa nje hewa yenye matone.** Hivyo, ni muhimu kukaa angalau mita 1 (hatua 3) kutoka kwa mtu mgonjwa.

Kwa hiyo ni muhimu kuosha mikono yako, kusafisha nyuso za vitu na kudumisha umbali wa kijamii kuzuia kuenea kwa magonjwa.

Sasa nitaelezea KUJITENGA KIMWILI / KIJAMII:

- Hivi sasa, moja ya hatua za haraka na ya muhimu ambayo familia yako yote inapaswa kuchukua **ni kujiepusha kukutana na makundi ya watu na mikusanyiko kiujumla, na pia hafu kama harusi, mazishi, sikukuu za kuzaliwa nk.**
- **Kwa hivyo tunapaswa kudumisha umbali wa angalau mita 1 kati yako mwenyewe na mtu yeyote anayekohoa au kupiga chafya.** Kwa nini? Mtu anapokohoa au kupiga chafya, wanatoa

nje matone madogo madogo kutoka kwenye pua au mdomo wao, ambayo yanaweza kuwa na virusi. Kama upo karibu sana, unaweza ukayavuta matone hayo kwa njia ya hewa, pamoja na virusi vya COVID-19 kama mtu anayekohoa anaugonjwa huo. Hii ni muhimu katika kumlinda kila mtu katika familia yako na haswa wale ambao wanaweza kuwa katika hatari zaidi kama wale wenye magonjwa sugu.

- Hii ni muhimu kwa sababu inasidia kuilinda familia yako lakini pia **inasaidia kuzuia maambukizi ya COVID-19** kuilinda jamii kwa ujumla, **kwa njia hii pia hatuilemei mifumo ya kiafya.**
- Hii inamaanisha kwa mfano mwanafamilia mmoja anaenda kununua chakula na anapotoka anaweka umbali kati yake na wengine na kujitahidi kutokusimama na wengine katika foleni kwa mfano wakati wa kulipia chakula.
- Kama una watu wenye hali hatarishi katika familia yako na unaweza ukapata namna ya kuwaweka mbali kimwili na kijamii hiyo itakuwa vyema zaidi, kama haiwezekani jitahidi kuzingatia kanuni za msingi za usafi.
- Kumbuka kwa sababu baadhi ya watu hawaonyeshi dalili zozote za COVID-19 wanaweza wasifahamu tayari wameathirika na kuendelea kusambaza kwa watu wengine waliohatarini zaidi, hii ndio maana kujitenga kijamii ni msingi hata kama unajihisi kuwa sawa. COVID-19 ina “kipindi maalumu” kati ya muda wa kupata virusi na muda wa kuanza kuonyesha dalili za ugonjwa. Makadirio mengi ya kipindi hichi kwa upande wa COVID-19 unaanzia kutokea siku 1-14, mara nyingi zaidi ndani ya siku tano.

Sasa nitaelezea dalili zinazoweza kuwa za COVID--19, dalili kuu zinahusisha:

- (1) 😞 Homa
- (2) 🤧 Uchovu
- (3) 🙅 Kikohozi kikavu
- (4) 🙅 Upumuaji wa shida

- **Homa, uchovu, kikohozi kikavu.** Wagonjwa wengine wanaweza kuwa na uchungu na maumivu, mafua, maumivu ya koo au kuhara.
- Dalili hizi **kikawaida ni za mwanzo na huanza pole pole.**
- Watu wengine huambukizwa lakini hawaonyeshi dalili zozote na hawajisikii vibaya.
- **Watu wengi (karibu 80%) hupona ugonjwa huu bila kuhitaji matibabu maalum.** Karibu mtu 1 kwa kila watu 6 ambao hupata COVID-19 huwa mgonjwa sana na hupata shida ya kupumua.
- **Wazee, na wale walio na matatizo ya kiafya** kama shinikizo la damu, shida za moyo au kisukari, **wana uwezekano mkubwa wa kuugua sana.** Watu wenye homa, kikohozi na shida ya kupumua wanapaswa kutafuta matibabu.
- **Ikiwa haujisikii vizuri, ni muhimu kwamba uwasiliane na namba maalumu iliyotolewa na Wizara ya Afya 76-592699 na watakuzeza pia jinsi ya kufikia huduma ya afya iliyo karibu wakati wakipunguza uwezekano wa wewe kueneza ugonjwa huo.**

Sasa nitaelezea orodha ya TAHADHARI za kuchukua hasa kuhusu kuwalinda wengine katika kaya yako:

- Ikiwa mtu ndani ya nyumba ni mgonjwa tafadhali hakikisha unawasiliana na mtoaji wa huduma ya afya kuuliza juu ya kupata dawa zaidi. Fafanua kwamba japo inaweza kuwa vigumu kupata, wahimiza kuwasiliana na mtoaji wa afya kwa njia ya simu ikiwa inawezekana, au uwasaidie kumfikia mtoaji wao wa huduma ya afya kupitia rufaa. Ni muhimu kuwa na dawa zao za kutosha endapo watahitajika kubakia nyumbani kwa muda mrefu.

Kumbuka: Kama familia haijaweza kupata huduma za msingi za kiafya, tafadhali andika na uijumuishe kwenye orodha ya rufaa kwenda kwa watendaji wa afya katika jamii. Tafadhali pata idhini yao, na uwasilishe kwa msimamizi wako au mtu anayehusika katika shirika lako (kwa ajili ya rufaa)

-Tafadhali muda wote tumia taarifa zinazoaminika kutoka kwenye maswali na majibu ya Shirika la Afya Duniani: <https://www.who.int/news-room/q-a-detail/q-a-coronaviruses> **au taarifa za Shirika la Afya Duniani za kupinga upotoshaji:** <https://www.who.int/emergencies/diseases/novel-coronavirus-2019/advice-for-public/myth-busters>

-Tafadhali kumbuka kwamba taarifa zote za msingi, nyenzo za Elimu na Mawasiliano (IEC) zinaandaliwa kwa ajili ya mlipuko wa COVI-19 nchini Lebanon ambao unawalenga watu wakubwa na watoto pia katika COVID-19 Dropbox ya ulinzi wa mtoto

-Tafadhali kumbuka asasi yako ikihitaji muongozo wa ziada kwa ajili ya wasimamizi wa kesi za ulinzi wa mtoto, tafadhali wajulishe viongozi wa Kamati tendaji ya kitaifa ya usimamizi wa kesi za ulinzi wa mtoto:

- Sara.mabger@rescue.org
- Monica.Martinez@savethechildren.org

Au kiongozi wa kikundi kazi cha ulinzi wa watoto walio katika dharura:

- jatwi@unicef.org